
Pia wakati tangu tujinyakulie uhuru kusafirisha mifugo ni kama unasafirisha bidhaa haramu. Tunauliza sheria ibadilishwe ili kwamba kuna mifugo inasafilishwa bila kutatizwa kwa soko ambazo ziko katika Kenya zile soko ziliko nje ya Kenya. Pia ufugaji tunauliza itambuliwe na sheria kama njia ya maisha ya wafugaji na ni njia ya uchumi. Pia tuna-recommend kwamba centers ya kupima magojwa ya mifugo ziwekwe katika sehemu za wafugaji ili mahali ya kupima magojwa mpaka uende Nairobi, damu ya ng'ombe ipelekwe mpaka Nairobi hakuna mahali katika ufugaji inajulikana ng'ombe ni mgojwa.

Pia tunauliza wafugaji wa Kenya walindwe kutokana na wafugaji wa nchi majirani ambae wanaingiza mifugo yao katika Kenya na kuharibu soko zetu na kufanya sisi kushindwa kupata bei mzuri kwa mifugo. Pia hizi protected areas ambaye ni forests, may be ni mambo ya game reserves ziwe free kwa mifugo kulishwaa wakati wa ukame kwa sababu area hizi wafugaji wamelinda wanyama miaka nenda miaka rudi hata wakati hatukuwa na mambo ya KWS.

Wafugaji wamechungwa na ku-treasure wanyama na kuona wanyama ni muhimu kwa maisha yao. Sasa kwa sababu kuna idhara inaitwa KWS, ile resources yote inapatikana kutokana na wanyama ambaye wamechungwa na pastoral people wafugaji wapatiwe share ya ile resources inapatikana kutokana na wanyama wa pori. Ngamia itabulike kama chakula na itabulike kwamba ni source ya kupata maziwa na ni mnyama hadi wakati wa ukame. Wakati huu hakuna compensation inafanyiwa wafugaji wakati wanyama wa pori wana-attack mifugo ama hata wakati wenyewe wanauwawa na wanyama wa pori. Tunauliza sheria mpya i-compensate wafugaji wakati mifugo yao inauwawa na wanyama wa pori na wakati pia wafugaji wanauwawa na wanyama hawa.

Watoto wetu wakienda shule wanafundishwa mambo ya kahawa ambaye hawajawai kuona. Curriculum ibadilishwe ili watoto wafundishwe mambo ya mifugo.

Juu ya ardhi tunapendekeza kwamba ile area yote inakaliwa na wafugaji ifanyiwe survey na wapatiwe communal title deed. Hii

itasaidia kwa sababu watu wengi wanakuja wakisema wanataka kufanya maendeleo katika area na ni grabbing wanafanya wanawacha wafugaji bila ardhi ya kulisha mifugo kwa hivyo ni hatari sana kwa wafugaji. Ardhi ambaye inakaliwa na wanyama wa pori lazima i-benefit wafugaji directly. Gazetted areas yote, forests, game parks iwe chini ya wafugaji. Barabara zetu miaka nenda miaka rudi zimekuwa barabara baya tunauliza barabara zinakuja katika area za pastoralist ziweweke lami.

Telephone system irekebishwe kwamba katika sehemu zote tunaweza piga simu. Ile powers zinakuwa enjoyed by Minister of Local Government iwe reduced na hio powers ipatiwe viongozi waliochaguliwa na wananchi.

Mshahara wa MPs ipunguzwe kwa sababu ni juu sana. Na hata ule muda wa MPs ku-qualify kupata pension iwe ni baada ya ku-win election mara tatu. Hapana win election mara moja na anapata pension.

Tunauliza DDCs ziwe scrapped na badala yake constituency development committee ambaye inahusisha viongozi na mambo ya maendeleo itabuliwe katika constituency level.

Security ya wananchi wa pastoralist serikali iwajibike kikamilifu na wale watu wamepoteza maisha yao kwa sababu ya banditry kwa sababu ya shifta wamepotesha mali yao iwekwe kwa sheria serikali iweze kuwa-compensate.

Serikali ipeane lawyers wakati wowote watu wa pastoralist hawawezi kujilipia akiwa na case ya kujibu serikali iweze kuwapatia lawyers ya kuwatetea. Asante sana.

Com. Dr. Swazuri: Sawa former MP J.J Falana make your presentation

J.J. Falana: Bwana Mwenye Kiti ma-commissioners, mabibi na mabwana, mimi kabla ya kusema hata yale ya kurekebisha Katiba ya maoni yangu, pengine ningeanza na comment hapa. Civic education ile imefanyika hapa kuelimisha watu wetu hapa juu ya jambo ya Katiba au juu ya yale yanapaswa kubadilishwa, mimi nafikiri haijafanyika vile inavyopaswa kufanyika. Bwana Chairman ni mpaka ujue ile kitu unayo kama ni nzuri ama mbaya ndio unaweza kufikilia kuibandili. Sisi hata ile Katiba inatukabili na inatutawala leo uzuri na ubaya wake hatujui. Kwa hivyo pengine bahati ni ya kuwa nyinyi mnaokaa hapa kutusikiza ni wana sheria na ile lugha tutazungumza hapa maombi yetu ni ya kuwa mtaweka kwa lugha ya sheria ili iweze kuwa kitu ya maanani huko mbele. Kwa hivyo tunawaomba yeyote ile tutakayosema hapa tafadhali iwe inaambatana na mafunzo ama hivyo mpokee.

Jambo la kwanza – Elimu – Mambo ya elimu hapa kwetu hailingani na elimu ya Kenya mahali ingine kokote. Hii ni kusema Bwana Chairman, mtihani ule tunafanya bila shaka mmekuwa Illeret, mmekuwa loiyangalani, mmekuwa Diriib Gombo, mmekuwa Laisanis mmeona hali watoto wetu wanavyoishi ndani na kusoma. Sasa haki iko wapi kama mtihani ile mtoto anakaa Illeret anafanya ni mtihani ule ule mtoto anakaa Alliance anafanya, mtoto anakaa Kabarak anafanya, mtihani ni ule ule. Now

hardship na ile hali hawa watoto wameweza kupata mafunzo kuweza kufika wakati wa kufanya mtihani ni ya shida sana.

Mtoto anayesoma na sitima, mtoto alieyekula siagi na bread kuamka na yule hakupata yeyote na anaingia kwa darasa na Kenya inafanya mtihani wetu kuwa moja na tunatarajiwa tushindane na wale watu wanakaa kwa hio district. Bwana Chairman hakuna haki hapo hata kidogo mimi ningeomba na ningependekeza hapa Katiba iwekwe irekebishwe mtihani ile inafanywa na watoto wa huko na ile inafanywa kwetu kwa vile ni moja passmark yetu iwe ni tofauti kwa sababu hali yetu ya kusoma sio moja. Itakuwa ni haramu kama passmark ya mtoto wa huko ni 90% na halafu mtoto yule anasomea Ileret iwe pia ni 90% hakuna haki huko.

Kwa hivyo tupewe hio nafasi wakati wa ku-mark ma-exams pass mark ya watoto wa hardship area kwa sababu as the saying goes hapa kuna watumizi wa serikali wanapata allowance ya kuitwa hardship area maanake nini? Actually it is very contradicting wanapewa msahara extra na ile inayopatikana huko wafanyi kazi wa serikali wanapewa hardship allowance kwa sababu mahali ile wanaishi ni mahali pa taabu, ni hardship na ni shida and it is on the same breath italingana kwa sababu of that hardship we don't enjoy the same learning facilities. Kwa hivyo hio ni vizuri iambatane na hio na tupewe mark tofauti.

Wakati wa kuingia shule kuu, university, passmark ya ku-admit watu hii mambo ya A-, B- Bwana Chairman na vile nimesema hali ile tunasomea ni tofauti consideration passmark grade ya kuingia kwa university kwa watoto pande yetu ifanywe chini ili tuweze kufaidika kuingia kwa university.

Nitakuja kwa mpaka – mpaka, boundaries, boundaries ya district na ya province ile tunaishi naye inakuwa ni kwa manufaa ya Provincial Administration. Inakuwa ni poritical boundaries kwa sababu ya haja ya utawala. Mimi nasema hii Bwana Chairman nikiwa na a point in mind, Rift Valley Province imetoka corner ile ingine ya Kenya na kidole Rift valley province imeingia mpaka hapa Merile kwa boundary. Sasa wakati vituko yote inatokea na hapo ndio mahali kunakuwa na majambazi, kuna mahali barabara hawatumii kwa sababu Rift Valley does not need it, sisi tuko kwa Eastern, sasa tukiwa kwa Eastern barabara ikitoka Isiolo kidogo tu, tunaingia mahali inaitwa 'Archas Post' tunaabiwa ni Rift Valley. So we travel in Rift Valley all through mpaka tunakuja Marsabit district. (Interjection)

Sasa Bwana Chairman mara nyingi watu kutoka hapa, tukisafiri insecurity mahali ile tunatwangwa na majambazi na inakuwa tabu ni katikati ya Melile na mpaka Mlima Wamba na hio sehemu administratively inaingia Rift Valley Province. Chochote kitokee hapa DC wetu wa hapa, OCPD hana mamlaka uwezo ni kama tunapigwa na foreigners kutoka nchi ya nje na sio Kenya watu wanakufa hapa na tunaabiwa this is out of his jurisdiction ni Rift Valley. Imagine a hundred kilometers from here shida insecurity hapa mpaka iwe referred to Rift Valley, Nakuru headquarters inaenda huko. Kwa hivyo hii sehemu tunaosikana naye boundaries iwe irekebishwe na ile sehemu tunaambatana naye iingie kwa Eastern Province. Hii mambo ya Rift Valley Province, kidole kuingia mpaka ndani, hio kidole ikatwe.

Jambo la tatu, sisi watu wa mkoa wa Eastern Province na Bwana Chairman utashangaa nikisema namna hio, serikali ikiambiwa Eastern Province na hata wewe Chairman na Committee yako tukisema Eastern Province, Eastern Province ile jamii inaingia kwa kila mtu kila mtu straight away ni Wakamba na Wameru, Eastern province. Eastern Province inakuwa dominated na Wakamba na Wameru kwa bahati mbaya Isiolo, Marsabit na Moyale tumesukumwa chini ya Eastern Province chini ya Wakamba na Wameru, mali hatupati share yeyote. Sisi tunaomba province ya tisa itolewe sisi tuwe na independent province na hakuna sababu ndio tukubaliwe tupate province yetu kwa sababu kufananishwa iko kitu tunaita NFD Northern Frontier District ya zamani. Baada ya uhuru Northern District Bwana Chairman just to give you background, you know eneo hii zamani ilikuwa ni Isiolo, Mandera, Wajir, Garissa, Moyale na Marsabit six districts. Ilikuwa ni hio sita may be part of Turkana and Samburu. Now wakati wa uhuru Bwana Chairman, serikali ya Kenya iliona fit, iliona sawa i-reward Wasomali kwa sababu Wasomali walitisha walitoka Kenya waliungana na wenzao Somalia. Hio matisho ilifanya serikali ya Kenya kuwapa Somalia the North Eastern Province wilaya tatu tu. Mandera, Garissa na Wajir iwe province na hio ni haki sisemi wanyanganywe.

Kwa haki ile Wasomali wamepata huko hii serikali yetu haijaona kitu kutupatia the same number of districts, Moyale, Marsabit na Isiolo pia tupewe kwa sababu in all fairness kama ni mambo ya uchumi, kama ni mambo ya mihani, kama ni mambo ya wakati tunakaa kwa hii jangwa na tunafanywa tushindane na tunashare resources na wale watu wameendelea kutushinda kwa sababu tulikuwa close wakati wa ukoloni halafu share yetu inarudi na inawekwa chini ya wenzetu Wakamba na Wameru Bwana Chairman it is very unfair. Kwa hivyo this is a Constitutional requirement tunaomba province ya tisa iundwe na hio province ya tisa iwe ni Moyale, Marsabit, Isiolo, Samburu, Turkana. Wale nomadic pastoralist community wale tunafanana tuwe na province yetu kando. Barabara mambo ya -----

Com. Okoth-Ogendo: Pokot

J.J. Falana: Sorry hapana Pokot hatutaki, Pokot wakae huko.

Public: Waende wapi?

J.J. Falana: Pokot wakae kwa Rift Valley kwa sababu Pokot kwa hakika Pokot hata vile walivyo sasa hawako vimbaya kwa sababu wako ile main na major community ya Kalenjin. Pokot sisi tunawa-identify na Kalenjin so Pokot hata kama ni pastoralist hawana taabu kama sisi. Hatufanani na hatuwahitaji.

Com. Okoth-Ogendo: Two more minutes.

Barabara ----- I will try and push it in those so minutes. Barabara Bwana Chairman sisi tuko kwa what is supposed to be the Great Transafrican Highway. This Transafrican highway inatoka Cape Town, South Africa na inaenda Egypt mpaka Cairo. Ni aibu sana barabara hii inatoka Africa kusini mpaka kule Cairo, mahali ile haijapigwa lami ni kutoka Isiolo kwenda Moyale.

Hii ni kumaanisha hii serikali hakuna haja na sisi kabisa. Hata kama ni kwa heshima, hata kama ni kwa heshima ya jina ya Kenya, kujua hii Transafrican highway imepigwa lami kila mahali kilometer 500 ndugu yangu, kilometer 500 inakuwa shida kwa hii serikali ya Kenya kuweka lami? Leo tukisafiri kwa sababu ya ubaya ya barabara sisi tuna rudikwa pamoja na mbuzi, ng'ombe kwa sababu hakuna public transport ingine, you will be surprised pengine kama kuna namna ya kuwafanya m-test hio, hio helicopter ingewachwa muingie kwa hii ma-lorry muone vile tunaona. Bwana Chairman, tunasafiri kwa mbuzi na ng'ombe and that has been our life all through tunaenda na mbuzi na ng'ombe. Sisi naye si watu wa shida namna hio yote ati hatuwezi ku-afford bus moja kuja hapa, we have saloons for example I am not bragging mimi mwenyewe nina gari yangu kidogo inakaa hapa Isiolo, I can't enjoy it. I can't use it haiwezi pita lami, haiwezi kuja hapa, am I not in Kenya, am I not part of this country surely? Kama hio kilometer 500 tu inakuwa shida kwa serikali ya Kenya kupiga ni kusema serikali haitujali, kwa hivyo there is no equitable fair distribution of resources, tupigwe barabara lami. Bwana Chairman nitakimbia haraka.

Tunakuja kwa ardhi – land – Title Deed – sisi haki yetu ni moja hapa hasa huku constituency inakuwa ni part of national reserve na national park. Ni hivi majuzi tu tuliomba Rais 1994 wakapewa sehemu kidogo wale watu wanaishi kwa sasa ikasemekana hiyo iwe exercise itolewe kwa national park na watu waishi. That is not enough, sisi tunaomba hii serikali inaonekana inahifadhi na inaona manufaa zaidi kwa wanyama kushinda binadamu. Sisi tunachukuliwa kama wanyama kwa hivyo hii sehemu tumeishi na imewekwa national parks na national reserves, iondolewe sisi tupewe haki ya kumiliki hio ardhi na tupewe matitle deed tuweze kuishi hapo juu.

Ya mwisho, sitaki sana kusukuma, mimi naunga mkono vile huyu mwakilishi wa livestock amesema, kuongeza tu. KMC mahali tulikuwa tunapeleka chakula yetu kuwekwa canning nyama ya mkebe leo hakuna na ni aibu sana serikali ya Kenya hasa kwa jeshi yetu na kila kitu tuna-import nyama kutoka Botswana, nchi zingine za nje na hali tuna nyama, sasa hata kama hatuwezi kupeleka mpaka KMC sisi tunaomba tutengezewe abattoirs hata kama ni hapa kwetu kulikuwa na mpango ifanyike hapo kwa ili tuweze kuweka ng'ombe ni taabu sana ku-load ng'ombe, it is even cruel to animals unaweka kwa lorry kutoka Moyale, six hundred kilometers hakuna kula, hakuna kutoka kwa gari mpaka Dagoretti, siku tatu nne. Na ikifika imekosa nguvu, imekonda hata hatuna faida ya kufanya, so to save all that kama tungetengenezewa hapa mahali Fulani tuchinje nyama ipelekwe na gari ya barafu mpaka huko, tutajiona kama tuko Kenya.

Ya mwisho kabisa Bwana Chairman, last, security – this is very important, usalama. Sisi tunataka kulindwa maisha na mali vile wana Kenya wengine wanalindwa. Hali ya usalama na mambo ya usalama serikali imesindwa. Na serikali imesindwa there is a very clear example I will give you Bwana Chairman. Wakati unaona mtu ana-delegate kazi yake kwa mwingine hio ni alama ya kuonyesha umeshindwa. Security siku hizi hii lugha ya homeguard this will make me very unpopular but I will say it. Homeguards, taabu ile imetusumbua hapa, the Government is arming one community against the other. Hii taabu ya security yote inaletwa na serikali arming one community against the other.

We have the regular police Bwana Chairman am concluding, we have the APs, we have those personnels trained ya kuweza

kubeba silaha. Sasa kama leo jamii moja hapa, Waborana mimi nikisema tumepungukiwa na bunduki usalama ni baya nitaenda kwa police kwa serikali nitapewa bunduki ya kupiga nani, Rendile. Rendile wataona wamepungukiwa, serikali itawapa Rendile bunduki kupiga nani, Gabra, Gabra wamepungukiwa, Gabra watapewa kupiga nani, Now the same Government arming its civilians against each other kumalizana sasa surely I don't think that is a solution so serikali ichukue jukumu ya kutulinda na hii mambo ya kutupatia pocket arms ya kumalizana sisi kwa sisi ikome. Asante Bwana Chairman.

Com. Okoth-Ogendo: Kuna maswali hapa njoo. Mhesimiwa kule kwingine tumekuwa I think in Moyale in North Horr, Laisamis they say homeguards are very very useful and they want them institutionalized, formalised because they are doing a good job and stabilise security so I don't know how this will go with you. The other question is on title deeds, you want to be given title deeds individually or as community?

Translator: *Swali hili ambalo aliyekuwa mbunge wa Saku mhesimiwa J.J. ameulizwa ni kuwa kule kwingine mahali Ma-Commissioners wametembea pahali kama Maikona, Laisamis sehemu zingine wananchi wanasema homeguards wanafanya kazi nzuri sana, sasa JJ hapa anasema nauliza home guard iweze kupunguzwa ama serikali iangalie hiyo? Swali ingine ambayo ameulizwa J.J. ni kuwa mambo ya title deed may be J.J atajibu na jibu lake nitatafsiri here.*

J.J. Falana: Madam Commissioner ya home guards mimi nilikuwa nikisema, nasema na nitasema juu ya homeguards. Homeguards wamekuwa na maana kwa sababu serikali imeshindwa that is in absence of the Government performing its duty because it has failed kwa sababu serikali imeanguka imeshindwa ndio homeguard imechukua hio nafasi, kama kungekuwa na serikali ya kutulinda yani tuna army, tuna police, tuna AP kama hawa walikuwa wakifanya kazi yao hakuna haja ya homeguards. Kwa hivyo hata wenzangu wakikwambia homeguards ina maana huko kweli ina maana kwa sababu hakuna serikali ya kuwalinda.

Ya pili, hii mambo ya title deed, title deed hapa mimi sikuuliza title deed ya communal, title ile nimesema hapa ni ya mashamba mahali ile tumekuwa na ukulima hapa na imekuwa excise kutoka national reserve na national park ndio naomba zile zilizobaki ifanyike, survey imefanywa hapa lakini title deed moja, hakuna mkulima mmoja leo anaweza kudai ardhi ile aliyo naye ni yake halali, bado tunakaa kama ile hali ya wanyama. Kwa hivyo ile title deed ninauliza hapa ni ya mtu binafsi na plot ya mtu binafsi sio ya kikabila.

Prof. Okoth-Ogendo: On education, I was a member of the Koech Commission and we had about quotas, cut-off points and so on and we found a lot of people some of them from Kitale even from Nyanza in Turkana schools, passing out as Turkanas. Isn't there a better way of affirmative action rather than lowering cut-off point because we are going to get a lot of people coming in into your schools and pretending they are Rendilles and Gabras and so on to take your system.

Translator: *Bwana Chairman anauliza kuhusu mambo ya elimu. Amesema kuwa ameuliza kuwa elimu kama vile J.J.*

aliyosema passmark ya watoto wetu iwe chini, pengine kuna wengi watatoka sehemu zingine waweze kuingia hapa halafu waweze kukata watoto ya hapa. Maoni ya J.J. kuhusu hio swali.

Com. Okoth-Ogendo: If you lower the passmark wanafunzi hawa wakienda katika zile shule hata kama ni ya serikali inawachukua muda to pick up ili waweze kuwa katika kiwango kimoja na wale waliokuwa mashule mazuri. Hakuna njia ya kuweza kwamba serikali ifanye hizi shule na wanafunzi kwa njia kiwango ambacho kiko juu ili waweze kufanya vizuri na wapite kama wale wenzao?

Translator: *Bwana Commissioner tena anauliza kujibu Bwana Chairman*

J.J. Falara: Kujibu ya Bwana Chairman Bishop Commissioner, mimi nimewaonyesha condition na nyinyi wenyewe mmeona mkitembea kwa hakika with all honesty hamwezi kusema there is a fair level playing ground kwa mtoto anayekaa Ileret and then the exam is that you must sympathise with that community. Mwalimu na mwanafunzi anakaa huko mtihani ni ule ule tu imetengenezewa huko. Mtoto asiye na facility yeyote huko au kama ni minimal there is nothing.

Ile kitu haitakosa kuwafikia ni karatasi ya mtihani hiyo ipelekwe na ndege, ipelekwe na nini siku ya mtihani the education ministry will make sure this paper gets there. Kama vile wanahakikisha hio mtihani ifike serikali and education for that matter ingehakikisha tuwe na facilities ya kutosha ya kuambatana na Wakenya wenzetu, we have no complain. But as long as there is no that level play ground I think we stand to be considered, that is my point. Kama kuna wengine watatoka huko sehemu ya raha na waje waungane na sisi kula taabu hapa they are welcomed hata mkitaka kutoa watoto wenu hapo waje hapa.

Com. Dr. Swazuri: Dr. Hussein from Catholic University.

Dr. Hussein Hassan Golisha: Thank you very much Mr. Chairman. Hussein Hassan Golicha. Nafikiri nitaongea kwa lugha ya Kiswahili. Kitu cha kwanza Bwana Chairman ningependa kugusia mambo ya usalama lakini hii sitakalia sana kwa vile watu wengi wameongea juu yake. Usalama upande huu ni kitu muhimu sana hasa hasa katika district hii. Usalama huu mara nyingi huwa inaletwa na kitu ambacho kwa kimombo tunaita resource conflict, tunapigania vitu vichache. Kutatua mambo ya usalama hapa ningependa tuangalie sana mambo ya ardhi. Mambo ya ardhi tuangalie. Vipi tutaangalia? Vile tunavyogawanya ardhi katika sehemu kadhaa ya Kenya hasa hasa sehemu hii imewaondoa wenyeji yani local population. Ardhi inasimamiwa na civil servants ambayo wewe utasikia tu ardhi fulani hakuna. Tungependa sana Bwana Chairman mambo ya ardhi wenyeji wawe ndani wajue inaendelea namna gani.

Pia kuhusu usalama Bwana Chairman, ningeliza equity in the distribution of resources. Mara nyingi huwa ni umaskini unatufanya tupigane kwa hivyo ikiwa sisi pengine hatuna raslimali lakini ile raslimali kidogo tunayo iwe developed and iwe equal kwa kila mwana Kenya.

Ya pili ningependa kuguzia mambo mawili. Ya kwanza sehemu hii ya Kenya ambayo ina-include Northern Kenya yote imeachwa nyuma wakati wa ukoloni kwa sababu pengine hawakuwakubali kama sehemu zingine za Kenya pengine ni dini yao. Serikali ya Kenya ilipokuja vile vile iliwaacha nyuma watu hawa kwa vile bado hawajawakubali vile walivyokataa mwingersa ndivyo vile vile waliwakataa. Utakumbuka 1962 referendum kutokana na wilaya sita NDF tano ziliamua kwenda Somalia kwa hivyo ikawa ni kama punishment sisi tuwachwe nyuma, barabara, shule, hospitali kutusaidia kuuza mifugo yetu hakuna. Kwa hivyo tumebaki nyuma 40 years ya uhuru watu wengi hapa hawajui.

Ni vipi tutatatua mambo haya, watu wengi wametaja affirmative action hapa Bwana Chairman ningependa ku-disagree na Bwana J.J. kuhusu affirmative action na ni sababu hii. Miaka 40 tumesaidiwa kama dawa kijiko mbili mara moja ama mara tatu. Mambo ya quota system ya serikali kutupangia watoto wangapi wataenda national school, hatuna haja nayo kwa vile haitusaidii. Ni nini twataka? Tunataka tusaidiwe tuwe na mashule. Kwa kingereza tunasema hatutaki tupewe samaki, tunataka tufunzwe kushika samaki. Kwa vile ikiwa wewe utanipa samaki kuna kiwango utanipa kumi, utanipa mia moja utachoka lakini tafadhali unifunze kusika huyu samaki mimi nitasika milioni moja kwa hivyo hatuna haja ya quota system for life tunataka marshall plan ya kuondoa shida ambayo tunayo hapa tuwe sawa na Wanakenya wengine hatutaki marks ipunguzwe watoto wetu waende university for ever ndio mara ya kwanza punguza twende na 68 lakini tafadhali unisaidie nishike 70 kama mtoto kutoka Kiambu, na mtoto kutoka Nyanza. Quota system for ever hatutaki na ikiwa affirmative action iko iwe ni muda sisi tusaidiwe tuwe kama Wakenya wengine.

Ya tatu, mambo ya afya – Mambo ya afya ni kitu muhimu sana katika Kenya na wewe utakubaliana na mimi kwamba health services katika nchi hii ilianguka kitambo. Na mimi ningependa ku-suggest ya kwamba vile tunavyojaribu kufanya ndio haifai, serikali pengine haina uwezo wa kupatia kila mtu facility hii ya health. Kwa hivyo mimi nina-suggest tutele mambo ya health insurance katika Kenya ili kila mwana Kenya awe anahudumiwa na serikali kwa njia fulani hii tunaweza wale ambao wana uwezo wawe na insurance yao, wale ambao hawana uwezo serikali i-subsidice. Nina hakika tunatumia pesa mingi katika mahospitali ambao haitusaidii, hio ni mambo ya afya.

Pia ningependa kuguzia mambo ya serikali, je tunataka serikali ya aina gani, tunataka federal Government ama tunataka central Government. Hapa na nafikiri ninaongea kwa niaba ya watu wengi hapa, iwe central, iwe federal mimi nina haya ya kusema. Kitu cha kwanza central Government imeanguka, imeanguka in the sense that it has failed to supply us with services. This is known whatever they said they are to do for 40 years, most of it is not available. Free primary education, water by when, we are pushing it now to 2020.

May be what is best for Kenya is a federal Government. But here for the local people sisi hatutaki federal Government ambayo sisi hatuna namna ya kuiangalia. Yaani what I mean kuna conditions Fulani ziwe satisfied sisi tu-accept federal Government. Mimi nimesema central Government haina kazi, federal Government ni bora kwetu lakini sio federal Government jina, hivyo

ndio nasema. Kitu cha kwanza economy ya Kenya yote ziwe zinuliwe hata sehemu kama hii, what we need is a marshall plan ya kutuina sisi tuwe kiwango sawa na wengine halafu mtuambie on your marks-get set-go, halafu sisi tuone kama tutashindana na Wanakenya wenzetu au la.

So number one, condition ya kwanza jimbo yetu ama ile jimbo tuakuwako dani iwe imeendelezwa. Sisi hapa tuna mizigo, livestock industry iwe developed kama vile industry za kahawa huko central Kenya na chai huko Rift Valley na sugar huko Nyanza industry zetu ziwe developed. Infrastructure kama mhesimiwa

(inaudible interjection)

Thank you na kama vile J.J. alisema barabara hii tunataka infrastructure Mr. Chairman, tumendanganywa kwa miaka mingi ya kwamba maendeleo ndio inalete barabara. Hapa tunataka tuwe very clear, ni kuku ama yai ilikuja kwanza? Hio ni kutuzunguza ni yai ama ni kuku. Kuku ndiye alizaa yai, mayai ndio ilikuwa kuku, that is not the issue. Is it development ambaye inaleta barabara ama ni barabara inaleta development? Economists watatueleza hii. Sisi tukisema tunataka barabara mnasema mna nini huko ili barabara ijengwe? Mimi nilikuwa nafikili mjenge barabara ndio tuwe na hizo vitu. Kwa hivyo infrastructure lazima zinjengwe.

Kitu cha pili, ikiwa tutaenda majimbo national institutions zile ziko, national schools, universities, referral hospitals, air ports ziwe national assets zisiwe mali ya jimbo fulani ambayo asset iko. Kwa sababu gani? Mimi na wewe na sisi zote tuko hapa tumechangia ikiwa ni Kenyatta university saa hizi iko Thika ama Kiambu? Sio ati ni ya watu wa Kiambu ama hapo, mimi nimetoa kodi hawa wote wametoa kodi wakajenga. Kwa hivyo hizi major national assets ziwe ni national sio za jimbo.

Ya mwisho kuhusu hizo conditions lazima sisi tuchague na tuelezwe ni jimbo gani tunaenda, kama vile J.J. alivyosema na utanisamehe ninamtaja sisi ni semeji, kama vile J.J. alivyosema kutoka 40 years hii ya independent tumewekwa katika Eastern Province. Eastern Province kama alivyosema ni kubwa sana, sehemu hii Marsabit, Isiolo, Moyale tumesahauliwa sisi ni kama tortoise anayeshindana na hare wazi tunajua ni nani anashinda. Wewe utakumbuka hapa Machakos Kabaa High School was established in 1926 kama vile Alliance na Maseno. Sisi hapa Marsabit Secondary School ni 1966 watani-correct kama mimi sijasema ukweli. Je tutaweza kushindana vipi? Ikiwa ni kazi, ikiwa ni national resource ambao inagauliwa ni wale ambao wako juu. Hata nomination katika Kenya's Parliament imewahi kuja upande huu wa Eastern Province? Sisi tumeachwa nyuma kwa sababu hatuwezi kushidana an wale. Tungependa sana tuwe na ninth province na jina nitakupa Northern Province ambaye itatufanya tushidane na wao, WaTurkana tutashidana na wao vizuri, Wasamburu tutashidana na wao vizuri.

Com. Okoth-Ogendo: Can you summarise?

Dr. Hussein Adam: I am summarizing. Ningependa kuguzia mambo ya election hasa hasa election ya President na

ningependa kutaja ya kwamba kitu ambacho kimetugawanya sana kikabila ni election ya President. Serikali nyingi za nje ambazo zimekuwa na demokrasia kwa muda mrefu kuliko sisi kama Wingereza, kama Ujeremani, kama India mambo ya direct election ya mtukufu Rais hakuna kwa vile ikiwa ni Mjaluo atasimama hapo Wajaluo zote tutapiga foleni. Ebu Boranaa mmoja ajitokeshe nitasimama President, utakuta zote tuko nyuma yake. Kwa nini unatulazimiza tuwe na ukabila kama hio? Let us not elect a President directly, wacha tuchague wajumbe tuwe katika Bunge halafu the head of that party ambaye imeshida a-form Government. Huyu President awe ceremonial tu wa kukaribisha wageni wa serikali lakini sio wa power ambayo niliyosema.

Ya mwisho Bwana Chairman, unaonekana umeniharakisha kidogo nitamalizia nikisema sisi economy yetu ni ya mifugo na sisi tungependa kitu cha kwanza ministry ya serikali ziwe fixed sio ati leo kumi na tano na kesho ishirini na saba ziwe fixed. Na katika hizi ministries sisi tungependa ministry ya livestock development na kitabo kidogo ilikuwako, leo hakuna, leo hatuna hio ministry ya livestock development. Sisi tunataka hio ministry iwe hapo na isiwe tu department ya Ministry of Agriculture pahali pengine wanasema Ministry of Coffee and Tea, sisi hatuhusiki. Kwa hivyo tunataka tuangaliwe hio ministry ikuweko na tuweze kusaidiwa. Thank you very much.

Com. Okoth-Ogendo: Tunatengeneza Katiba sasa na ule muudo wa serikali na umesema ungependa muudo wa serikali ya majimbo lakini umepeana conditions ambazo ni lazima zifanywe kabla ya hio serikali kama ni mambo ya infrastructure, industries and so forth. Hivi ni kusema unasema kwamba katika Katiba hii tutengenezayo basi tutaendelea na muudo mwingine mpaka mpate mambo hayo ili twende regional what do you mean?

Dr. Hussein Adam: This is what I mean. Number one and I will say this again that the system as we have has left us behind, we are not in a position to compete. So if we are going to have majimbo, then we will have it on those conditions so that again we are not completely left out. If you create majimbo of Eastern Province today so that you have eight majimbos as it were based on the provincial boundaries, then we are still a rose is a rose by other name. What is the difference kama tulikuwa tunakaliwa bando tunakaliwa, kwa hivyo tunasema kama tutaenda majimbo tafadhali sisi nasi tuje juu.

Com. Baraza: These ministries, you have a number yourself in mind that how many ministries we could have?

Dr. Hussein Adam: I would suggest it should be between 15 and 17 because at one time as I remember we had ministry for rural development, ministry of water, ministry of whatever there are very many ministries which we can combine because we are spending so much money on 27 ministries, 27 ministers, 27 Permanent Secretaries, 54 Deputy Secretaries and the following staff and how many houses do we maintain in Nairobi when we are using 27 ministries?

So if it is a Constitutional requirement that we look at it we say we need a ministry of education, we need a ministry of finance, we need something of economic planning or whatever then we have a certain limited number which we can manage so that we do not become an employer whose job is just to pay the employees. You hear in Kenya here most of the time we are talking

about we can't pay salaries but your job is not to pay salaries, your job is to give services. You should have just enough people to run the job. That was my (inaudible)

Com. Okoth-Ogendo: Thank you I am going to ask you, if you and your colleagues can expound on the idea of marsahall plan for Northern Kenya, the Member of Parliament for Moyale addressed us at length on that but I think it is important we have very clear ideas and a document which we can look at as a Commission. So if you can take that one up yourself and develop it and send it to us in Nairobi, it will be extremely useful before we start that item.

Com. Dr. Swazuri: Thank you very much. Northern NGO development forum.

Bonaya Bonkale: Kwangu sasa mimi nakuja kutoa maoni si kuomba, mimi sijakuja kuomba serikali nilikuja kutoa maoni kwa Constitution of Kenya Review Commission. Kwa hivyo naomba maoni ile tunatoa iingie katika Constitution ya Kenya. Mimi naanza na preamble tunaanza na sisi tuko wakabila 42 katika Kenya na mimi nataka wakabila 42 yote itambuliwe. To be recognized as people, kuwa Wakenya haina maana peke yake lazima watu desturi yao kabila yao itambuliwe ndiyo wawe watu wa maana.

Na ya pili katika wilaya ya Marsabit, Welfare Monitoring survey conducted in 1994 ilionyesha Marsbit district ni maskini mwisho katika Kenya nzima ikiwa na 88.2% below poverty line ikifuatiwa na Samburu 84.2% kwa nini sisi tulikuwa maskini? Mambo yale yalitufanya maskini tuliwekwa katika serikali kuu central government na maoni yangu ni sisi tuwe regional government. Region mimi na-propose ni Marsabit na Moyale and Isiolo iwe jimbo moja na hio jimbo kwa nini iwe jimbo moja mimi nafikiria hivyo? Kwa sababu sisi sote tunatumia lugha moja na hio ituendeshe na ya pili lugha nafikiri lugha asili mia mingi ya wakaaji wa area hii hawajui Kiswahili nami nafikiri katika regional Government lugha Kiswahili isikuwe lugha ya hio jimbo ikuwe lugha ya wenyeji.

Na regional Government tuwe na governor na Provincial Administration ifutiliwe mbali kabisa kwa maana imeshidwa kutuhudumia na tunataka ma-elected leaders katika jimbo, representatives iwe councillors na iwe imepitishwa katika Katiba au tuwe na njia ingine tofauti. Lazima wawe heads of department, wawe executive officers macouncillors watu wale mamechaguliwa na raia ndio washikilie raslimali yote ya wananchi, sio mtu anatoka Kisumu in the name of head of department, Mombasa, Nairobi na hajui vile tunaishi hapa. Kwa hivyo wenyenji wale wanachaguliwa ndio wawe head of department, wawe executive officers wale wa technical person awe karani peke yake.

(Inaudible interjection) Kengele hio, ukizungumza Kiswahili pasha sauti ama mimi nita..

Bonaya Bonkale: Haya maoni yangu tulikuwa tunataka regional Government, Government ambaye wale wamechaguliwa na raia washikilie positions yote ya serikali katika regions na lazima wawe wenyeji sio wale wanatoka nje ya hio jimbo, wale

wanajau lugha ya mama, na wale wanafahamu maisha yote ya jamii katika eneo hilo. Kwa hivyo nilisema hatutaki watu wanaendesha maisha yetu wakiwa wanatoka Mombasa, Kisumu, Nyeri na hawajui taabu yetu, na hawajui hali yetu yote.

Na ya pili kulikuwa na titling – sisi ni pastrolists, pastrolism haijatabulika dunia mzima ya kwamba ni maisha ya heshima, ni maisha ya nidhamu ama ni maisha ambaye watu wanajielekesha inaonekana na wale wakulima ya kwamba ni maisha ya upumbavu, tunataka sheria itambue ya kwamba pastrolism, ufungaji ni njia kamili ni njia ya maisha kuendesha maisha. Kwa hivyo sheria itambue leo kwamba pastrolism is a real way of life not a retrogressive way of life.

Na ya tatu pia traditional system – Traditional system itambuliwe ya kwamba ndio inaendesha maisha hata zamani wazee ndio walikuwa wanaendesha maisha wanaangalia mifugo ndio wanachunga mali, wanachunga ardhi na malisho. Kwa hivyo trust land act ambaye ifanya ardhi yetu ishikiliwe na council kutoka leo irudishwe kwa wazee kwa wenyeji. Na kwa nini nasema hivyo, County Council ilikuwa inaokota senti ilikuwa inaokota pesa for example in Isiolo district inaokota million 98 na kutoka siku ile trust land ilianza 1937 mpaka wa leo hawajawai kuhudumia watu. Kwa sababu imeshindwa kuhudumia watu trust land itupwe mbali ardhi irudi kwa mikono ya wenyeji.

Na ingine pia ardhi mingi ikiwa na maji mzuri, malisho mzuri yote iliwekwa katika national reserve na game parks. Sisi tunataka national park, game reserves ambaye imenyakuliwa na County Council na serikali yote irudi kwa wenyewe kwa maana hakuna trickle down benefits kutoka hio tourism earnings mpaka leo hatujapata ardhi yoyote. Na iko act ambaye inasema mining act pia inasema land six feet below ni ya serikali, maji six feet ndio iko chini and mineral yote iko, mafuta yote iko kwa sababu hio kile kitu chote kiko chini ya ardhi irudishwe kwa mikono ya wenyeji kisheria.

Forests, game reserves, game parks na wanyama yote kwa sababu the national reserves, County Councils, the Central Government hawajahudumia, hawajaletea watu faida mpaka saa hii na walinyanyasa watu wakachukua ardhi yao na walisukuma wenyeji, pastrolists katika area ya jangwana. Kwa hivyo ardhi hio yote imechukuliwa na jina ya game reserves, forests yote irudi na ifaidishe watu wakiwa hawa wanasimamia na desturi yao ya zamani.

Com. Okoth-Ogendo: Please summarise.

Bonaya Bonkale: I am summarizing. Mambo ya central Government, service delivery. Serikali ya Kenya was signing conventions, international conventions agreement, they rectified, wali-assess kwa pahali mingi sana hapa duniani. Walisema sisi tunapatia nyinyi maji safi, tutapatia nyinyi njia, chakula walisema hivyo na kwa kabisa na kwa destuli na kwa kisheria serikali lazima ituhudumie sisi na hio njia zote ya kupatia sisi salama na kuhudumia vile Wakenya wengine walihudumia kwa maana sisi ni wale ambao wanalipa kodi. Kodi billion mia mbili Kenya ina-budget kila siku hata sisi tunalipa, hatujui kwa nini highland ya Kenya inakuwa tarmac, education yote iko pande hii tunaachwa.

Kwa hivyo sisi tunataka serikali hio conventions yote iwe domesticated into Constitution of Kenya today iwe under fundamental rights. Bill of right iwe expanded hizo rights yote iwekwe kwa sheria sheria ya leo ituangalie sisi kabisa kwa maana sisi tuliachwa na kisheria hatujapata share yetu kutoka the consolidated fund revenue ya serikali yote ile ilikotwa mwaka hii yote ndio hatujapata huduma. Nafikiri tukipata regional Government sisi tunataka serikali igawanye mali na raslimali yote ya pori kwa jimbo na tujiendeshe na siku hiyo tutatosheka.

Na ya mwisho kabisa eneo hili mambo ya ajabu ilifanywa Bwana Chairman, tafadhali one minute. Mambo ya ajabu ilifanya serikali ya Kenya ilitesa watu. There is what we call adjacent district, and Eastern Province and adjacent districts contain where wakati watu waliwekwa in camps in Isiolo district they put people in three camps. There is Malkamari massacre, there is Wagala massacre, whereby during those times between 1964 na 1968 the police officer aka-shoot anybody on sight so people here are destroyed by security forces in this system through bad laws. So sisi tunataka serikali kwa sababu hawa ndio walitunyanya, waliumiza watu ndio walifanya wao maskini na fukara tunataka serikali iweke affirmative action so that we want a Constitution redress tuangaliwe ndio tushikane na wale wenzetu kule Kenya highland wale wameendelea. Na mimi nashukuru hivyo. For that pastrol development mimi nataka Ministry of Pastrol Development to directly redress our marginalisation.

Na ya tatu Kenya iweke department of civic education Wakenya wote wafunzwe juu ya serikali ilioundwa na itakaeundwa. Asante mimi nashukuru.

Com. Dr. Swazuri: Nafasi hii tunapea Mhesimiwa Abdi Tari Sasura who is Assistant Minister for Energy.

Hon. Abdi Tari Sasura: Thank you Mr. Chairman, first and foremost wacha nichukue nafasi hii kuwakaribisha nyinyi Ma-Commissioner kwa hii eneo la wakilishi wa Bunge ya Saku. Ya pili wacha niwapongeze nyinyi wale mlikuja Marsabit. Bwana Mwenye Kiti, mimi jana na juzi nilikuwa Isiolo na nilikuwa disappointed na ningependa nyinyi pia mjue mkirudi na Commission yenu ikikaa pamoja ikuwe registered. Observation yangu ambaye nili-observe Isiolo, I was very disappointed when I heard that your Commissioners who were in Isiolo went to do some work in Modogashe and the following day walikuwa waende wafanye kazi Garbartula which is between Modogashe and Isiolo. Na badala ya kulala Modogashe na kwenda kufanya kazi Garbartula walisema sisi watuwezi kulala Modogashe.

Walitoka Modogashe wakalala Isiolo halafu wakatoka Isiolo wakakuja kazi Garbartula, kuonyesha ya kwamba Modogashe hakuna binadamu wanalala ama Garbatula hapana mahali binadamu analala. Mimi napongeza nyinyi kuja Marsabit nasikia mmeenda (inaudible) nasikia mmeenda Dukana nasikia mmeekula mbuzi na mmeekula hardship. So wale wameenda Isiolo I am sorry to say Githu Muigai and Lethome have disappointed us completely. Now having said that Mr. Chairman, I want to thank you for giving me unlimited time to give my proposals. Mr. Chairman nitajaribu kufupisha, I have a written memorandum and I assure you I am not going to read it I am just going to highlight one or two points and present it.

Com. Okoth-Ogendo: Take seven minutes.

Hon. Abdi Tari Sasura: Seven and a half minutes. Mr. Chairman kitu cha kwanza, jambo ya kwanza nataka kuanza naye ni jambo ya citizenship, uraia wa Kenya. Bwana Mwenye Kiti mimi ningependa kwanza kupendekeza ya kwamba nani swali inaulizwa, nani who is supposed to be a Kenyan citizen? Ningependa kupendekeza ya kwamba mtu yeyote ambaye anazaliwa Kenya awe Kenyan citizen. Nasema hivi kwa sababu nataka kuwapatia tu mfano hapa tu Marsabit. Tumekuwa na wakati wa Regime ya Haile Sellasie ilianguka tulikuwa na watu waliotoroka kutoka huko, wakakuja wakaishi hapa. Wakaoa jamii ya hapa halafu wakazaa watoto na hawa watoto wanaambiwa nyinyi si Wanakenya. They are not allowed to get identity cards, nilikuwa nime-discuss this na Principal Immigration Officer na akasema ya kwamba hawa watoto kwanza they apply wakuwe Kenyan citizen na mtoto ambaye ni mu-Ethiopia sawa, amekuja ameo hapa, hana mbele wala nyuma, ile kitu anaye ni hapa Kenya tu. So I want it to be a requirement that anybody born in Kenya is a Kenyan citizen.

Ya pili, I want to address the issue of dual citizenship – And in this regard Mr. Chairman I want to refer to this book, it is a compilation of Kenya Human Right Commission and this is a revised edition imeandikwa the year 2000, inaitwa the forgotten people.

Mr. Chairman may be you have not seen the forgotten people, these forgotten people were not forgotten by their mothers, they were not forgotten by their fathers, they were not forgotten by their children, they were forgotten by the Constitution of Kenya. Mr. Chairman, it is important that we have dual citizenship especially in Northern Kenya for one reason. That, sisi wale tuko hapa border district, wale tuko border district in Northern Kenya, it is a fact whether it will be denied or whether it will be overlooked or whether it is assumed, it is a fact that, (interjection) mimi naongea lugha yoyote mchanganyiko. It is a fact Bwana Chairman sisi wale tunakaa northern district tunaishi Kenya lakini jamii wetu wako Ethiopia. Tunaishi Kenya lakini jamii yetu wako Somalia wale wanaishi Mandera. Nataka kukupatia mfano moja hapa Bwana Chairman, hii apana fiction, hii ni facts mwaka wa 1999 tarehe 22 mwezi wa June kulikuwa na mkutano wa Borana inaitwa Gumigayo, ambayo ilifanywa huko Ethiopia na hii jamii wamekaa Ethiopia na wamepitisha sheria hio ni kama Bunge yao, Bunge ya WaBorana ambayo inakaa na mtu asikundanganye hata sisi tunafuata hio Bunge yao tukiwa hapa.

